## JARIDA KWA AJILI YA WAPOKEAJI NA WATUNZAJI

## IDHINI YA MATUMIZI YA DHARURA (EUA) YA CHANJO YA PFIZER-BIONTECH YA COVID-19 YA KUZUIA UGONJWA WA VIRUSI VYA KORONA 2019 (COVID-19) KWA WATU WENYE UMRI WA MIAKA 16 NA ZAIDI

Unapewa Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19 ili kuzuia Ugonjwa wa Virusi vya Korona 2019 (COVID-19) unaosababishwa na SARS-CoV-2. Jarida hili lina taarifa itakayokusaidia kuelewe hatari na faida za Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19, ambayo huenda unawea kupatiwa kwa sababu kwa sasa kuna janga la COVID-19.

Chanjo hii ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19 inaweza kukukinga dhidi ya COVID-19. Hakuna chanjo iliyoidhinishwa na Shirika la Chakula na Dawa la Marekani (FDA) ya kuzuia COVID-19.

Soma Jarida hili kwa taarifa kuhusu Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19. Zungumza na mtoa chanjo ikiwa una maswali. Ni uamuzi wako kupewa Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19 au la.

Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19 ni dozi inayomezwa mara mbili, huku moja ikitolewa baada ya wiki tatu, kwenye msuli.

Huenda Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19 isimkinge kila mtu.

Jarida hili linaweza kuwa limesasishwa. Ili kupata Jarida lahivi karibuni, tafadhali angalia www.cvdvaccine.com.

### JE, UNATAKIWA KUJUA NINI KABLA YA KUPEWA CHANJO HII?

### JE, COVID-19 NI NINI?

Ugonjwa wa COVID-19 unasababishwa na virusi vya korona vinavojulikana kama SARS-CoV-2. Aina hii ya virusi vya korona haijawahi kuonekana hapo awali. Unaweza kuambukizwa COVID-19 kwa kukaribiana na mtu mwingine mwenye virusi hivyo. Huu ni ugonjwa wa mfumo wa upumuaji hasa unaoweza kuathiri viungo vingine. Watu wenye COVID-19 huripotiwa kuwa na dalili mbalimbali, kuanzia dalili ndogo mpaka ugonjwa sugu. Dalili zinaweza kutokea kuanzia siku 2 mpaka 14 baada ya kuambukizwa virusi. Dalili zinaweza kuwa ni pamoja na: homa au baridi; kikohozi; kushindwa kupumua; uchovu; maumivu ya msuli au mwilini; maumivu ya kichwa; kupoteza ladha au hisia ya kunusa; mwasho wa koo; kujaza uoevu au kutokwa kamasi; kichefuchefu au kutapika; kuhara.

### JE, CHANJO YA PFIZER-BIONTECH YA COVID-19 NI NINI?

Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19 ni chanjo ambayo haijaidhinishwa ambayo huenda ikazuia COVID-19. Hakuna chanjo iliyoidhinishwa na FDA ya kuzuia COVID-19.

FDA imeidhinisha Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19 itumiwe kwa dharura ili kuzuia COVID-19 kwa watu wenye umri wa miaka 16 na zaidi chini ya Idhini ya Matumizi ya Dharura (EUA).

Kwa taarifa zaidi kuhusu EUA, angalia "**Je, Idhini ya Matumizi ya Dharura (EUA) ni nini?**" mwisho mwa Jarida hili.

### JE, UNAPASWA KUMWAMBIA NINI MTOA HUDUMA YA CHANJO WAKO KABLA YA KUPEWA CHANJO YA PFIZER-BIONTECH YA COVID-19?

**Mwambie mtoa huduma ya chanjo kuhusu hali yako yote ya kiaya, ikiwemo kama:**

- una mizio yoyote
- una homa
- una matitizo ya kuvuja damu au unameza dawa za kuzuia damu kuganda
- una kinga dhoofu au unameza dawa inayoathiri mfuno wako wa kinga
- una mimba au unapanga kuwa na mimba
- unanyonyesha
- umepata chanjo nyingine ya COVID-19

**JE, NANI ANAPASWA KUPATA CHANJO YA PFIZER-BIONTECH YA COVID-19?**
FDA imeidhinisha Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19 itumiwe kwa dharura kwa watu wenye umri wa miaka 16 au zaidi.

**JE, NANI <u>HAPASWI</u> KUPATA CHANJO YA PFIZER-BIONTECH YA COVID-19?**
Hupaswi kupata Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19 ikiwa:

- uliathiriwa vibaya sana baada ya kumeza dozi ya chanjo hii
- uliathiriwa vibaya sana na kiungo chochote cha chanjo hii

**JE, CHANJO YA PFIZER-BIONTECH YA COVID-19 INA VIUNGO GANI?**
Chanjo ya Pfizer BioNTech ya COVID-19 ina viungo vifuatavyo: mRNA, lipids ((4-hydroxybutyl)azanediyl)bis(hexane-6,1-diyl)bis(2-hexyldecanoate), 2 [(polyethylene glycol)-2000]-N,N-ditetradecylacetamide, 1,2-Distearoyl-sn-glycero-3-phosphocholine, na cholesterol), kloridi ya potasiamu, monobasic potassium phosphate, kloridi ya sodiamu, dibasic sodium phosphate dihydrate, na sukrosi.

**JE, CHANJO YA PFIZER-BIONTECH YA COVID-19 HUPEANWA VIPI?**
Utadungwa sindano yenye Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19 kwenye msuli.

Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19 ni dozi inayomezwa mara mbili, huku moja ikipeanwa baada ya wiki 3.

Ukipokea dozi moja ya Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19, unapaaswa kupokea dozi ya pili ya hiyo chanjo baada ya wiki 3 ili ukamilishe chanjo.

**JE, CHANJO YA PFIZER-BIONTECH YA COVID-19 IMESHATUMIWA HAPO AWALI?**
Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19 ni chanjo ambayo haijaidhinishwa. Katika majaribio ya kliniki, takriban watu 20,000 wenye umri wa miaka 16 na zaidi wamepokea angalau dozi 1 ya Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19.

**JE, CHANJO YA PFIZER-BIONTECH YA COVID-19 INA FAIDA GANI?**
Katika jaribio la kliniki linaloendelea, Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19 imezuia COVID-19 baada ya dozi 2 iliyopeanwa baada ya wiki 3. Kipindi ambacho unakingwa dhidi ya COVID-19 haijulikani kwa sasa.

**JE, CHANJO YA PFIZER-BIONTECH YA COVID-19 INA HATARI GANI?**
Athari za kimatibabu ambazo zimeripotiwa za Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19 ni pamoja na:

- maumivu kwenye sehemu ulipodungwa sindano
- uchovu
- maumivu ya kichwa
- maumivu ya msuli
- baridi
- maumivu ya viungo
- homa
- sehemu ulipodungwa sindano kuvimba
- sehemu ulipodungwa sindano kuwa nyekundu
- kichefuchefu
- kuhisi vibaya
- kuvimba kwa tezi za limfu (limfadenopathi)

Kuna uwezekano mdogo kwamba Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19 inaweza kusababisha athari mbaya sana. Mara nyingi athari mbaya sana hutokea ndani ya dakika chache hadi saa moja baada ya kupata dozi ya Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19. Dalili za athari mbaya sana ni pamoja na:

- Kushindwa kupumua
- Kuvimba usoni na kooni mwako
- Mapigo ya moyo ya haraka
- Vipele sugu mwili mzima
- Kizunguzungu na unyong'onyo

Huenda hizi zisiwe athari zote za kimatibabu zinazoweza kutokea kutokana na Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19. Athari mbaya sana na zisizotarajiwa za kimatibabu zinaweza kutokea. Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19 bado inachunguzwa kwenye majaribio ya kimatibabu.

**JE, NINAPASWA KUFANYA NINI KUHUSU ATHARI ZA KIMATIBABU?**
Ukiwa na athari mbaya sana, piga simu 9-1-1, au nenda kwenye hospitali iliyo karibu sana.

Mpigie simu mtoa huduma wako wa chanjo au mtoa huduma wakowa afya ukiwa na athari zozote za kimatibabu zinazokusumbua au zisizokwisha.

Toa taarifa ya athari za kimatibabu kwenye **Mfumo wa Kutoa Taarifa ya Athari Mbaya za Chanjo wa FDA/CDC (VAERS)**. Nambari ya VAERS ya bila malipo ni 1-800-822-7967 au toa taarifa mtandaoni kwenye https://vaers.hhs.gov/reportevent.html.

Tafadhali jumuisha "Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19 EUA" kwenye mstari wa kwanza wa kisanduku cha #18 cha fomu ya kuripoti.

Isitoshe, unaweza kutoa taarifa ya athari za kimatiibabu kwa Pfizer Inc. kwa kutumia taarifa ya mawasiliano iliyotolewa hapo chini.

| Tovuti | Nambari ya faksi | Nambari ya simu |
|---|---|---|
| www.pfizersafetyreporting.com | 1-866-635-8337 | 1-800-438-1985 |

**JE, ITAKUWAJE IKIWA NITAAMUA KUTOPATA CHANJO YA PFIZER-BIONTECH YA COVID-19?**
Unaweza kuamua kuchanjwa au kutochanjwa Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19. Kuamua kutochanjwa hakutaathiri, au kubadilisha huduma yako ya kawaida ya afya.

**JE, KUNA MACHAGUO MENGINE YANAYOPATIKANA YA KUZUIA COVID-19 MBALI NA CHANJO YA PFIZER-BIONTECH YA COVID-19?**
Kwa sasa, hakuna chanjo mbadala iliyoidhinishwa inayopatikana ya kuzuia COVID-19. FDA inaweza kuruhusu chanjo nyingine ya kuzuia COVID-19 itumike kwa dharura.

**JE, NINAWEZA KUCHANJWA CHANJO YA PFIZER-BIONTECH YA COVID-19 PAMOJA NA CHANJO NYINGINE?**
Hakuna taarifa inayohusu kutumia Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19 pamoja na chanjo nyingine.

**JE, ITAKUWAJE IKIWA NINA MIMBA AU NINANYONYESHA?**
Ikiwa una mimba au unanyonyesha, jadili machaguo yako pamoja na mtoa hudumawako wa afya.

**JE, CHANJO YA PFIZER-BIONTECH YA COVID-19 ITANIAMBUKIZA COVID-19?**
Hapana. Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19 haina SARS-CoV-2 na haiwezi kukuambukiza COVID-19.

**WEKA KADI YAKO YA CHANJO**
Utakapopewa dozi yako ya kwanza, utapewa kadi ya chanjo ya kukuonyesha siku ya kurudi kwa ajili ya dozi yako ya pili ya Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19. Kumbuka kubeba kadi yako utakaporudi.

**TAARIFA YA ZIADA**
Ikiwa una maswali, tembelea tovuti au piga simu kwa namabri ya simu iliyotolewa hapo chini.

Ili kupata Jarida la hivi karibuni, tafadhali tambaza msimbo wa QR uliotolewa hapo chini.

| **Tovuti ya kimataifa** | **Nambari ya simu** |
|---|---|
| www.cvdvaccine.com | 1-877-829-2619<br>(1-877-VAX-CO19) |

**JE, NINAWEZAJE KUPATA MAELEZO ZAIDI?**
- Muulize mtoa huduma ya chanjo.
- Tembelea CDC kwenye https://www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/index.html.

- Temblea FDA kwenye https://www.fda.gov/emergency-preparedness-and-response/mcm-legal-regulatory-and-policy-framework/emergency-use-authorization.
- Wasiliana na idara yako ya afya iliyo karibu au ya jimbo.

**JE, TAARIFA YANGU YA CHANJO ITAREKODIWA WAPI?**
Mtoa huduma ya chanjo anaweza kujumuisha taarifa yako ya chanjo kwenye Mfumo wako wa Taarifa ya Chanjo (IIS) ya mamlaka ya ndani au ya jimbo au kwenye mfumo mwingine ulioteuliwa. Hii itahakikisha kwamba utapata chanjo sawa utakaporudi kwa ajili ya dozi ya pili. Kwa taarifa zaidi kuhusu IISs tembelea: https://www.cdc.gov/vaccines/programs/iis/about.html.

**JE, MPANGO WA FIDIA YA KUZUIA JERAHA NI NINI?**
Mpango wa Fidia ya Kuzuia Jeraha (CICP) ni mpango wa serikali unaoweza kulipia gharama za kimatibabu na gharama nyingine mahususi za watu fulani ambao wamejeruhiwa vibaya na dawa au chanjo fulani, ikiwa ni pamoja na chanjo hii. Kwa kawaida, lazima madai yawasilishwe kwa CICP ndani ya mwaka mmoja (1) kuanzia tarehe uliyota chanjo. Ili kupata maelezo zaidi kuhusu mpango huu, tembelea www.hrsa.gov/cicp/ au piga simu namba 1-855-266-2427.

**JE, IDHINI YA MATUMIZI YA DHARURA (EUA) NI NINI?**
FDA ya Marekani imeifanya Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19 ipatikane chini ya utaratibu wa upatikanaji unaoitwa EUA. EUA inaungwa mkono na azimio la Katibu wa Afya na Huduma kwa Wanadamu (HHS) kwamba hali zilizopo zinahitaji tutumie dawa na bidhaa za kibiolojia kwa dharura wakati wa janga la COVID-19.

Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19 haijakaguliwa kwa njia sawa na bidhaa ya FDA iliyoidhinishwa na kuthibitishwa. FDA inaweza kutoa EUA wakati ambapo vigezo fulani vimetimizwa, ikiwa ni pamoja na kutokuwa na mbadala zinazopatikana, zinazotosha au zilizoidhinishwa. Isitoshe, uamuzi wa FDA unategemea uthibitisho wa kisayansi unaoonyesha kwamba huenda bidhaa inaweza kuzuia COVID-19 wakati wa janga la COVID-19 na kwamba faida zinazojulikana na zinazoweza kuwa za bidhaa ni nyingi kuliko hatari zinazojulikana na zinazoweza kusababishwa na bidhaa. Lazima vigezo hivi vyote vitimizwe ili kuruhusu bidhaa itumike katika matibabu ya wagonjwa wakati wa janga la COVID-19.

EUA ya Chanjo ya Pfizer-BioNTech ya COVID-19 inatumika katika kipindi cha azimio la EUA la COVID-19 linalotoa sababu halali za kutumia bidhaa hizi kwa dharura, isipokuwa kama zimesitishwa au kubatilishwa (ambapo huenda bidhaa zisitumike tena).

Pfizer

Imetengenezwa na
Pfizer Inc., New York, NY 10017

BIONTECH

Imetengenezwa kwa ajili ya
BioNTech Manufacturing GmbH
An der Goldgrube 12
55131 Mainz, Germany

LAB-1451-1.0

Imesahihishwa: Desemba 2020

Scan to capture that this Fact Sheet was provided to vaccine recipient for the electronic medical records/immunization information systems.

Barcode Date: 12/2020